Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Nebraska, Idara ya Ulemavu wa Kimaendeleo

# Medicaid Waivers kwa Ustahiki wa wakazi wa Nebraska

NEBRASKA
Good Life. Great Mission.

## Huduma kuhusu Waivers za Nyumbani na za Kijamii

Huduma za Medicaid waiver za Nyumbani na za Kijamii (HCBS) zina ruhusu majimbo kutumia fedha za Medicaid kwa kutoa huduma kwa watu ambao wanaishi na ulemavu ndani ya nyumba zao na jamii, ambao vinginevyo wangehudumiwa katika taasisi. Vituo vya Huduma za Madicare na Medicaid (CMS) vina kubali waivers toka kwa taasisi. **Mtu anapaswa kupokea Medicaid ili awezekuwa na waiver.** Kushiriki kwenye Medicaid HCBS Waiver ni kwa hiari na inahusu mtu binafsi.

Kuwa na ustahiki wa Medicaid HCBS waivers*yoyote* , ni lazima:

1) Uwe raia wa Marekani au mgeni aliye kuwa na ustahiki chini ya Uhamiaji wa shirikisho na Sheria ya Uraia na kuwepo kisheria nchini Marekani;
2) Kuwa mkazi kisheria wa Jimbo la Nebraska; na
3) Kupokea Medicaid.

Kila waiver ina ustahiki wake ambao unahitajika. **Mtu anaweza kuwa kwenye waiver moja maramoja tu**, hatakama wanaweza pokea huduma kwenye waiver moja wakati ambao husubiri waiver nyingine kupatikana kwao.

Kuna waivers mbili za kuhudumia watu wanao ishi na ulemavu, ambao wana timiza Kiwango cha Kituo cha Uuguzi (NF) na wanapenda kupokea huduma na msaaada ndani ya jamii zao:

- **Msamaha wa Wazee na Walemavu (AD):** **Kwa watu wa rika zote ambao wana ulemavu na watu zaidi ya miaka 65. Imekusudiwa kusaidia watu kuishi nyumbani.**
- **Jeraha kwa Ubongo (TBI) Waiver**: Kwa watu wa miaka 18 na zaidi ambao walipata jeraha kwa ubongo. Waiver hii si kwa ajili ya kuumia kwa ubongo kwa sababu ya kiharusi, uvimbe, au sababu zingine zisizo za jeraha la ubongo. Inalenga kusaidia watu wa TBIs kuishi nyumbani.

Kutakuwa waivers tatu kuhudumia watu wa ulemavu wa ukuzi, ambao wanatimiza Nafasi ya Utunzaji wa Kati kwa Watu wa Ulemavu wa Akili (ICF-IID) Kiwango cha Uuguzi.

- **Waiver ya Ugonjwa wa Ulemavu wa Ukuzi (CDD)** Inatoa huduma za ushiriki ndani ya jamii na usaidizi kwa makazi mchana. Kwa kuzingatia kufundisha ujuzi wa maisha huru ndani ya yumba ya mtu. Waiver hii ni kwa watu wa miaka yote hatakama huduma za mchana zianakuwepo kwanzia umri wa miaka 21.
- **Waiver ya Siku ya Watu wa Kubwa wenye Ulemavu wa Ukuzi (DDAD)**: Inatoa huduma za ushiriki ndani ya jamii na usaidizi kwa makazi mchana na ushirikisho, pamoja na msaada kikazi au mafundisho ya ujuzi wa ajira ijayo. Waiver hii ni kwa watu wa umri ya miak**a**21.
- **Waiver ya Msaada kwa Familia (FSW)**: ***Waiver hii inatarajia kuanza mwanzo ya 2024.*** Itatoa huduma na msaada kwa kusaidia watoto wa Ulemavu wa Ukuzi ili waendelee kuishi na familia nyumbani. Waiver hii itakuwa kwa watu kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka 21.

## Jifunze Zaidi

- Nini na hitaji ili kujua kuhusu Medicaid? - Nini wahitaji na washiriki wanahitaji kujua.
- Laha ya habari kuhusu Waiver ya Umri na Ulemavu- Maelezo ya ukurasa moja ya huduma za AD Waiver na mahitaji.
- Waiver ya Laha ya Habari kuhusu Jeraha kwa Ubongo- Maelezo ya ukurasa moja ya huduma za TBI Waiver na mahitaji.
- Waiver ya Laha ya Habari kuhusu Ugonjwa wa Ulemavu wa Ukuzi- Maelezo ya ukurasa moja ya huduma za CDD Waiver na mahitaji.
- Laha ya Habari kuhusu Waiver ya Siku ya Watu wa Kubwa wenye Ulemavu wa Ukuzi - Maelezo ya ukurasa moja ya huduma za DDAD Waiver na mahitaji.

**Rasilimali zote zinapatikana kwenye:** http://dhhs.ne.gov/Pages/DD-Resources.aspx.

**Rasilimali nyingi zinapatikana ndani ya lugha zingine kwenye:** https://dhhs.ne.gov/Pages/DDD-Resources-In-Foreign-

- Waiver ya Msaada kwa Familia (FSW) Laha ya Habari (INAKUJA) – *Inatarajiwa mwaka 2024.* Maelezo ya ukurasa moja ya huduma za FSW na mahitaji.

| HUDUMA ZINAZOTOLEWA KWA KILA WAIVER | AD | CDD | DDAD | FSW* | TBI |
|---|---|---|---|---|---|
| **Siku ya Watu wakubwa** hutoa shughuli za kijamii, ushunguzi, na msaada. Hakuna mafunzo. | | ✓ | ✓ | | |
| **Siku ya Afya kwa Watu wa kubwa** inaruhusu muundo wa kijamii, mafunzo, na shughuli za afya. | ✓ | | | | ✓ |
| **Usaidizi kwa Maisha** hutolewa na taasisi zenye leseni kwa huduma za makazi na usaidizi. | ✓ | | | | ✓ |
| **Usaidizi wa Teknolojia** hutoa vifaa vya kuongeza ustadi wa kila siku na kujitegemea. | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| **Mafunzo ya Uuguzi** ni elimu bila malipo toka kwa watunzaji. | | | | ✓ | ✓ |
| **Siku ya Uhamasishaji wa Mtoto**hutoa mafunzo na msaada kwa watoto katika mazingira ya jamii. | | ✓ | | ✓ | |
| **Kazi** husaidia kwa kazi za nyumbani ili uweze kubaki nyumbani. | ✓ | | | | ✓ |
| **Ushirikiano wa Jamii/Miunganisho** husaidia mtu kufikia jamii yake. | | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| **Mwenzi** kwa watu wazima wa umri wa miaka 18; uchunguzi na misaada ya kijamii hutolewa kwa nyumba ya mtu na kwenye mazingira ya jamii. | ✓ | | | | ✓ |
| **Tathmini ya Ushauri** kwa watu wakubwa hutoa tathmini na mapendekezo kwa changamoto za tabia. | | ✓ | ✓ | | |
| **Siku ya Usaidizi** hutoa shughuli na kufundisha ndan ya eneo la mtoa huduma. | | ✓ | ✓ | ✓ | |
| **Tathmini ya Marekebisho kwenye Mazingira** huamua mabadiliko ya nyumba au gari ambayo yanaendana na mahitaji yako. | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| **Matunzo ya ziada kwa Watoto wenye Ulemavu** kwa vijana wenye umri wa miaka 17 inaruhusu muuguzi wa kawaida kuajiriwa au kuhudhuria shule. | ✓ | | | | |
| **Ushauri wa Familia na Wenzio** huwapa washauri uzoefu wa maisha kupitia mifumo inayoongoza na rasilimali. | | | | ✓ | |
| **Nyumbani Tena/Huduma za Mapito** hulipa mara kwa mara gharama zisizo za usanidi ili uweze kutoka kwa taasisi na kuhamia kwa nyumba ya kibinafsi au kusaidiwa kwa maisha. | ✓ | ✓ | ✓ | | |
| **Vyakula Vyakupeleka Nyumbani** hukupa vyakula nyumbani kwako. | ✓ | | | | ✓ |
| **Ugeuzi wa Nyumba na Gari** kwa makazi yako binafsi au gari la msingi kutosheleza mahitaji yako, baki salama, na kufanya vitu peke yako. | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| **Mfanya kazi wa nyumba** hufanya shughuli za nyumbani na huduma ya nyumbani kusaidia mlezi wa kawaida wakati hawapo au hawawezi kusimamia nyumba yao. | | ✓ | | ✓ | |
| **Kujenga Ustadi wa Kujitegemea** hutoa mafunzo katika shughuli za maisha ya kila siku kusaidia na ujuzi uliopotea. Hutolewa kwa nyumba yako au kwa mpangilio la kundi. | ✓ | | | | |
| **Uhamasishaji Ndani ya Nyumba** hutoa mafunzo kwa nyumba yako binafsi (Kujitegemea Maisha) au familia nyumbani (Usaidizi wa Maisha kwa Familia). | | ✓ | ✓ | ✓ | |
| **Kujitunza binafsi** kwa watu wa kubwa wa umri wa miaka 18, pamoja na usaidizi wa shughuli za maisha ya kila siku, huduma za mwenzi, na kazi zinazo husika na afya. | ✓ | | | | ✓ |
| **Mfumo wa Jibu la Dharura Kibinafsi (PERS)** hutoa shauri kuita msaada. | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| **Kabla ya kazi** hufundisha ustadi wa kawaida ambao unahitajika kwa kupata kazi. | | ✓ | ✓ | | |
| **Uhamasishaji kwa Nyumba** katika mpangilio wa kutoa huduma; ni pamoja Nyumba Kuendelea, Nyumba ya Mwenyeji, na Kuishi Pamoja. | | ✓ | | | |
| **Pumziko** hutoa utulivu kwa muuguzi wako wa kawaida. | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| **Msaada wa Kitaalamu kwa Kundi Ndogo** katika biashara au jami, ambapo unajifunza ujuzi wa kazi na tabia kwa ajira ijayo. | | ✓ | ✓ | | |
| **Utaalamu wa Uhamasishaji kwa Nyumba** kwa watu wa kubwa ambao hawawezi kutoka kwa nyumba zao katika siku za huduma nipamoja na | | ✓ | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Matibabu na Tabia. | | | | | |
| **Ajira Inayosaidiwa – Kibinafsi na Kwa uchunguzi** kukusaidia kuwa na ushindi, kazi za ushirikisho. | | ✓ | ✓ | | ✓ |
| **Uwezeshaji wa Matibabu kwa Nyumba** ni huduma inayo eleweka katika mpangilio wakutoa huduma, hupatika wakati una yote mbili DD na ujonjwa mbaya wa akili. | | ✓ | | | |
| **Usafirishaji** hutoa usafiri katika maeneo ya jamii yako kwa madhumuni yasiyo ya matibabu. | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |

**Huduma kwa FSW zina tegemea taasisi kukubali na ni chini ya mabadiliko.*